Wiki Hii

# UTUMISHI

Julai 27, 2026 // Toleo Maalum // Ofisi ya Rais - Utumishi // ps@utumishi.go.tz



## RIDHIWANI: DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050 IWE AJENDA KUU YA KILA SIKU



Watendaji Wakuu wa Taasisi, Mashirika ya Umma na Wakala za Serikali wameagizwa kuhakikisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 unakuwa sehemu ya majukumu yao ya kila siku kwa kuoanisha mipango, bajeti na maamuzi ya Taasisi wanazoziongoza na malengo ya maendeleo ya Taifa.

Agizo hilo limetolewa Julai 24, 2026 Kibaha mkoani Pwani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete, wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa Watendaji Wakuu yaliyolenga kuimarisha uongozi na utendaji wa Taasisi za Umma.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Ridhiwani amewakumbusha Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma kuwa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ulianza rasmi Julai Mosi mwaka huu, hivyo wanapaswa kuhakikisha agenda hiyo inaakisiwa katika utekelezaji wa bajeti, vipaumbele na mipango mkakati ya taasisi zao ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Amesisitiza kuwa mafanikio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 hayatapatikana kwa matamko pekee, bali kupitia maamuzi ya kila siku yatakayofanywa na viongozi wa Taasisi.





Aidha, amesema kila bajeti, mradi, uwekezaji na huduma inayotolewa inapaswa kuonyesha mchango wake katika kufanikisha malengo ya Dira 2050.

Sambamba na hayo, amewataka kuhakikisha viashiria vya utendaji vya taasisi zao vinaendana moja kwa moja na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ili kurahisisha upimaji wa mchango wa kila Taasisi katika utekelezaji wa Dira hiyo kila mwaka na kuimarisha uwajibikaji katika utumishi wa umma.

"Nina imani kuwa maarifa na uzoefu mlioupata utatafsiriwa katika utendaji wenye matokeo chanya, hivyo kuimarisha utawala bora, kuongeza ufanisi wa Taasisi-za Umma na kuharakisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa manufaa ya maendeleo endelevu ya Taifa," amesema Mhe. Ridhiwani.

Katika kuhitimisha mafunzo hayo, Mhe. Ridhiwani aliipongeza Ofisi ya Msajili wa Hazina, Taasisi ya Uongozi na wadau kwa maandalizi na uratibu wa mafunzo hayo, akieleza kuwa yamewajengea uwezo wa kuongoza Taasisi kwa ufanisi, kuongeza tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.





# Qwaray aonya Watendaji wanaokwamisha Stahiki za Watumishi, asisitiza ufanisi E-utendaji kufikia dira 2050



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Regina Ndege Qwaray (Mb), ametoa onyo kwa Wakurugenzi, Maafisa Utumishi na Wakuu wa Idara katika taasisi za umma wanaochelewesha kuwasilisha nyaraka za malimbikizo na fidia za watumishi.

Amesema Serikali haitasita kuchukua hatua za kisheria na kiutawala dhidi ya mtendaji yeyote atakayebainika kuwa kikwazo cha watumishi kupata haki zao kwa wakati.

Akizungumza katika kikao kazi cha kusikiliza changamoto za watumishi wa umma kilichofanyika Halmashauri ya Mji Mbulu, Mhe. Qwaray amesema Serikali imekuwa ikipokea malalamiko kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya malimbikizo na fidia za watumishi.

Uchambuzi umebaini kuwa baadhi ya madai hayo hayafikishwi kwa wakati Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya uchambuzi na taratibu za malipo kutokana na uzembe wa baadhi ya watendaji" amesema.



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Regina Ndege Qwaray (Mb) akizungumza na Watumishi wa Halmashauri ya Mji Mbulu wakati wa kikao kazi cha kusikiliza changamoto za watumishi wa umma na kujadili namna ya kuboresha utendaji kazi.*

Aidha, Mhe. Regina amesisitiza kuwa Serikali tayari imeshatenga fedha kwa ajili ya kulipa stahiki hizo, hivyo hakuna sababu ya watumishi kuendelea kucheleweshwa kupata haki zao kutokana na urasimu unaoweza kuepukika.

Katika hatua nyingine, Mhe. Qwaray amesema mafanikio ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 hayawezi kupatikana bila kuwepo kwa amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa, hivyo amewasisitiza watumishi wa umma uwa mabalozi wa amani, kutoa huduma kwa usawa-bila ubaguzi na kujenga imani ya wananchi kwa Serikali kupitia utendaji wa haki, weledi na uwajibikaji.

Akizungumzia matumizi ya teknolojia katika utumishi wa umma, amesema tangu mwaka 2024 Serikali imeanza kutumia Mfumo wa e-Utendaji katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha utendaji wa kila mtumishi unachangia moja kwa moja katika utekelezaji wa malengo ya taasisi na vipaumbele vya Taifa.



Hata hivyo, amesema tathmini ya hivi karibuni imeonesha kuwa bado kuna changamoto ya kutounganishwa kwa majukumu ya watumishi na mnyororo wa matokeo ya kitaifa, jambo linaloathiri uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya kazi.

utokana na hali hiyo, Mhe. Qwaray amewataka watumishi wa umma kutumia kikamilifu dirisha la kuanzia Julai 15 hadi 28, 2026 kuandaa na kuwasilisha Mipango ya Utendaji ya Mwaka wa Fedha 2026/27 kupitia Mfumo wa e-Utendaji.

Zoezi hilo lisichukuliwe kama utaratibu wa kawaida bali kama hatua muhimu ya kuhakikisha kila lengo la mtumishi linaendana na mwelekeo wa maendeleo ya Taifa" amesema.







# Rais Samia amuapisha Prisca Lwangili kuwa Naibu katibu Mkuu Utumishi



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan akimuapisha Ndugu Prisca Burton Lwangili kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye hafla iliyofanyika Ikulu ya Tunguu Zanzibar, tarehe 27 Julai, 2026.*





*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb) ameshiriki katika ufunguzi wa semina elekezi ya Viongozi kuhusu umuhimu wa mawasiliano serikalini iliyofunguliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan , Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Julai 28, 2026 Ikulu Tunguu, Zanzibar.*



Ofisi ya Rais
Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora

*Salamu za Pongezi*

# BI. PRISCA LWANGILI

Hongera kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.



Tunakuahidi ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yako.